# INFORMASJON OM SOSIALHJELP - SWAHILI

## Taarifa kuhusu msaada wa jamii

Msaaada wa fedha wa kijamii ni mapato ya muda ambayo inapewa kwa kusaidia kulipa gharama muhimu ya kuishi na ya nyumba. Lengo ya msaada huu ni kukusaidia upate uwezo wa kujihudumia mwenyewe haraka iwwezekanavyo.

Ni lazima utumikishe fursa zingine zote kabla ya kustahili msaada wa kijamii. Inaweza kuwa kwa mfano, kupitia kazi, mapato mengine ama fedha zako mwenyewe. Ikiwa unahitaji kujua ni fursa gani unayo, unaweza kuwasiliana na ofisi ya NAV kwa ushauri na mwongozo.

### Kabla ya kuomba msaada

Unapotuma ombila lako, inakufaa kueleza kuhuusu wewe mwenyewe na hali yako ya ki fedha. Lazima ueleze vile vile kimsingi hali iyo kupitia vitambulisho unapotuma ombi lako. Ikiwa umeolewa, una shurti ya kueleza kuptitia vitambulisho hali ya ki fedha ya mwenzi wako. Vifwatayo ni mfano ya vitambulisho unwezwa kuulizwa:

- Marejesho ya kodi
- Salio ya ma akaunti yote ya benki
- Mapato (kwa mfano: hati ya malipo, misaada mengine, msaada ya Watoto…)
- Mkataba wa kupangisha nyumbani ya kuishi
- Chekechea / mazowezi ya kisha shule
- Makutano na mtoto

Mtu yeyote ana haki ya kuomba usaidizi wa kifedha wa kijamii, na kupata uthatmini ya binafsi. Unaweza pia kutuma ombil la kupata «taarifa, ushauri na mwongozo”, bila kujali kama una haki ya msaada wa kifedha wa kijamii. Fomu ya kuomba usaidizi huu inapatikana ku www.stange.no/nav

### Fursa nyingine

- Chunguza kama una haki ya usaidizi ya malipo ya nyumba kutoka kwenye Husbanken. Fomu ya kuomba usaidizi huu inapatikana ku www.husbanken.no
- Tafuta kazi
- Malipo ya likizo, pesa ya ushuru, pesa ya watoto, msaada kwa watoto,

### Dharura

Ikiwa uko katika dharura, utapata jibu la haraka. Dharura inaamanisha ya kuwa huwezi kupata kitu unayohitaji kabisa, kama vile chaula, gharama za usafiri na gharama ya vifaa inayoweza kuzuia kuzimwa kwa huduma muhimu kama vile umeme.
Ikiwa uko katika dharura, utapata jibu la haraka.

**Gharma ya usafiri**

Viwango ya malipo ya kujihudumia vinakusudiwa kulipia gharama ya kusafiri. Ikiwa una gharama kubwa ya kusafiri, unaweza kuomba msaada wa ziada. Msaada wa kijamii haikusudie kulipa malipo ya leseni ya udereva ama ya gari lako mwenyewe, isipokuwa tu gharama hiyo ni ya muhimu kwako.

**Baada ya kuomba**

Muda wa uthatmini wa kesi hutofautiana. Ikichuguwa Zaidi ya mwezi mmoja, utapokea jibu ya awali. Ikiwa haujatoa viambatisho yote yenye kutambulisha hali yako, inaweza kuchugua muda mrefu kabla ya kupata jibu la ombi lako.

Tukimaliza kushugulikia ombi lako, utapokea uamuzi na jibu kutoka kwetu ambayo lazima uisome kwa umakini. Mara tuna madai moja ama Zaidi katika uamuzi, ambayo ni lazima utimize. Katika jibu yet ku ombi lako, kuna taarifa Zaidi kuhusu kiasi ya malipo na tarehe ya malipo itakayo fuata.

Ikiwa unaona ya kuwa uamuzi wetu si sahihi, unaweza kukata rufaa bado wiki tatu kupita kutoka wakati uliyo pokea uamuzi. Rufaa itatumwa ku ofisi ya NAV. Una haki ya kuagua kesi yako. Ijulishe ofisi ya NAV ikiwa umetaka.

**Lazima tuarifiwe kukiwa mabadiliko**

Ni lazima utuarifu ikiwa hali yako inabadilika baada ya wewe kutuma ombi lako. Kwa mfano, inaweza kuwa:

- **Unapata mapato ziada** kama vile mapato ya kulipwa manufaa ya mara moja baada ya kuzaa, pesa ya ukosefu wa ajira, marupurupu ya ulemavu, posho kuhusu ushiriki ya masomo ya lugha, zawadi, faida na Zaidi. Ikiwa mapato haitoki kwa NAV, lazima uwasilishe hati. Inabidi utumie pesa jinsi inayoweza kukusaidia kuishi na unapasha kuji hudumia mwenyewe kadri unayo weza.
- **Unatarajia kuhama**
- **Ikiwa umewekwa kwenye taasisi**. Kwa mfano hospitali, gerezani na kwenye taasisi ya matibabu
- **Ikiwa idadi ya watu unayeishi nao imebadilika**

**Watoto wa umri ya Zaidi ya miaka 18**

Watoto wa umri ya miaka 18 na Zaidi, lazima wajitengemee wenyewe kimsingi. Ikiwa wanaitaji usaidizi wa kijamii, watume ombi lao wenyewe isipokuwa tu wanasoma kwenye shule ya sekondari. Ikiwa una Watoto walio na umri wa miaka ya zaidi ya 18, na wanao soma ku shule ya sekondari, lazima ueleze katika ombi lako. Ambatanisha ombi lako na vitambulisho wa nyaraka ya ufadhili wa masomo kutoka mfuko wa mkopo.

**Kinacho lazimishwa kwako**

Ukiwa na umri miaka 30 kushuka chini, lazima ushiriki katika shughuli Fulani ili uweze kupokea usaidizi wa kifedha wa jamii, isipokuwa tu kuna sababu nzuri kwa nini huwezi kushiriki. Unaweza kulazimishwa vile vile kushiriki kwenye mazowezi hata ukiwa na miaka ya kupita miaka 30. Kama una fursa ya kufanya kazi, unatakiwa kuomba kazi. Ikiwa lengo ni wewe kupata kazi ama shughuli, basi unatakiwa kutuma kadi ya ripoti na uwe na ushirikiano kikamilifu na NAV.

## Viwango

Usaidizi wa kifedha umehesabiwa baada ya tathmini ya kesi ya mutu binafsi. Ofisi ya NAV inatumia ushauri wa serkali kwa ajili hali ya maisha ili iweze kujumuisha kiasi ya usaidizi unaye hitaji kwa kuishi. Viwango vinaweza kupatikana ku www.nav.no/satser . Kisha bonyeza ku "statlige veiledende retninsjer for økonomisk stønad".

Gharama inayotajika kwa ajili ya nyumba, umeme, afya, tiba ya shida ya meno na zaidi, ni tofauti na kwa iyo haiya jumuishwa katika kiwango kilichopendekezwa. Unaweza kutuma maombi ya msaada kuhusu swali haya ikiwa unahitaji. Unaweza pia kutuma maombi ya usaidizi kwa kulipa gharama ya watoto, kwa mfano gharma ya shughuli za mazowezi ya kisha shule, vyombo, kushikiana na Zaidi.

## Kanuni

Ni lazima ukuwe na kibali ya makazi wa halali nchini Norway kabla ya wewe kukubaliwa usaidizi wa ki fedha wa kijamii. Hauna haki ya kupata usaidizi huo ikiwa unakaa nje yan chi.

Kwa kawaida unapaswa tuma ombi yako ya usaidizi ku ofisi ya NAV inayopatikana katika manispaa unayoishi. Ukipokea manufaa ingine ya kijamii baadaye, ofisi yetu inaweza kudai malipo ya usaidizi wa kijamii uliopokea kwa muda huo kwa ajili yako na la mwenziwe hatimaye.

Unatuma ombi yako ya msaada wa kijamii kupitia tovuti ya www.nav.no/sosial. Hapo unaweza pia kutuma hati zako baadaye na kupata taarifa Zaidi kuhusu kazi ya Huduma wa kijamii na sheria iliopo. Utapata vile vile nyaraka ya sheria ya Huduma ya Jamii inayofafanua jinsi sheria inapaswa kueleweka.